**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GEM**

102/3
**KISWAHILI**
Karatasi ya 3
Julai/Agosti 2016
**Muda: Saa 2½**

**SEHEMU YA A : USHAIRI**

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1.
Haki ya mtu thawabu kuidai sitasita
Hata 'nipatishe tabu muhali mimi kukita
Kulitenda la wajibu liwe hai au mata
Nitafanya majaribu na inapobidi matata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

2.
Haki ya mtu u'ngwana siseme mimi nateta
Sitaukiri ubwana na jeuri unoleta
Na ikiwa ni kuwana sitajali sitajuta
Sikiri kuoneana na kupakana mafuta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

3.
Haki ifukie chini ipige na kuibuta
'Tumbukize baharini 'tazamia kuifwata
Ukaifiche jangwani nitakwenda kuileta
Itundike milimani nitawana kuileta
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

4.
Haki ijengee ngome izungushe na kata
Na fususi isimame iwe inapitapita
Tainuka nishikame haki yangu kukamata
Sifa kubwa mwanamume kuenda huku wasota
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

5.
Uungwana siuuzi kwa njugu au kashata
Ahadi za upuuzi na rai kuitaita
Kwa kila alo maizi hawi mithili ya bata
Tope yake makaazi na chakula cha kunata
Haki yangu 'taidai hata iwe ni kwa vita

**Maswali**

a) Bainisha dhamira ya mshairi. (alama 2)
b) Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
c) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 5)
d) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)
   i) Idadi ya mishororo
   ii) Mpangilio wa vina
f) Fafanua toni ya shairi hili (alama 1)
g) Taja nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
h) Tambua na ueleze maana ya mshororo ufuatao
   Mleo wa ubeti wa mwisho. (alama 2)

**SEHEMU B : TAMTHILIA**

**Mstahiki Meya : T. Arege**

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** "Duniani kuna watu na viatu na Cheneo ina watu na viatu."

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b)** Kwa kutoa mifano mwafaka, fafanua undani wa kauli ya msemaji. (alama 6)
**c)** Onyesha sifa za msemaji wa kauli hii pamoja wa umuhimu wake katika tamthilia. (alama 10)

**3. a)** Jadili mambo ambayo yanachanjia kuanguka kwa utawala wa Meya. (alama 10)
**b)** Eleza njia ambazo Wanacheneo walitumia katika kuleta mabadiliko katika Mji wa Cheneo. (alama 10)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**SEHEMU C : RIWAYA**
**Kidagaa Kimemwozea : K. Walibora**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Nina furaha kukujulisheni kwamba ... mnamo mwisho wa mwezi. Naomba mradi ... usitishwe ..."
- **a)** Weka mambo haya katika muktadha wake. (alama 4)
- **b)** Kuna dhana anayoikataa katakata msemaji wa maneno haya. Itaje na ueleze japo kifupi. (alama 2)
- **c)** Dhana hii inaonekana kukita mizizi katika jumuiya ya Wanatomoko. Dhihirisha. (alama 14)

**5.** Ndoa ni asasi ambayo kwayo mwanamke amedhulumika pakubwa katika jamii. Jadili kwa mujibu wa riwaya hii. (alama 20)

**SEHEMU D : HADITHI FUPI**
**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**
**Walibora K. na Mohamed S.A - Wahariri**
**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** Katika hadithi 'Ndoa ya Samani' "Sikutaka kuelezwa jambo la ziada. Nilitamauka kabisa kiasi cha kwamba tulipokuwa ..."
- **a)** Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- **b)** Kuna sababu iliyotolewa baadaye kama chanzo cha kutibuka kwa jambo hili. Itaje. (alama 2)
- **c)** Taja na ueleze sifa zozote tatu za mnenaji wa maneno haya (hapo juu) (alama 6)
- **d)** Eleza kinaganaga maudhui yanayojitokeza katika hadithi hii. (alama 8)

**7. a)** Ubaguzi ni kati ya masuala mazito yanayojadiliwa katika "Damu Nyeusi". Thibitisha. (alama 10)
- **b)** Ushirikina umedhihirika wazi katika hadithi 'Glasi ya Mwisho Makaburini'. Tetea dai hili kwa maelezo na mifano mwafaka. (alama 10)

**<u>SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI</u>**

**8. a)** Ngano ni nini ? (alama 2)
- **b)** Eleza sifa zozote sita za ngano. (alama 6)
- **c)** Vyanzo vya ngano vina umuhimu gani ? (alama 5)
- **d)** Tofautisha kati ya mighani na ngano za mashujaa. (alama 4)
- **e)** Ngano za kiayari zina umuhimu gani katika jamii zetu ? Taja tatu. (alama 3)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479